TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Usajili na matumizi ya majina ya vikoa vya .tz (.tz domain names)

Jina la kikoa cha nchi kwa matumizi ya mawasiliano kwa njia ya Intaneti linawakilishwa na herufi mbili zinazoitambulisha nchi kwa mfano **.**za (Afrika Kusini), **.**zw (Zimbabwe), **.**ke (Kenya) na **.**tz (Tanzania). Tanzania Network Information Centre (tzNIC) ni kampuni isiyotengeneza faida iliyopewa jukumu la kusimamia na kuendesha rajisi ya majina ya vikoa vya .tz. Mojawapo ya majukumu ya tzNIC ni utoaji usajili wa majina ya vikoa vya .tz kwa watu binafsi, taasisi na mashirika yanayotoa huduma au yanayofanya biashara nchini Tanzania. Hivyo basi mashirika ya Kitanzania yanahamasishwa kusajili majina ya vikoa kama vile xyz.co.tz kwa ajili ya utambulisho wa moja kwa moja, ulio pekee, wenye kujibainisha na kuhusishwa na Tanzania badala ya majina ya vikoa kama vile xyz-tanzania.com ambayo yana ubainishaji usio wa moja kwa moja na wa wazi.

Hatua ya kwanza ya kutoa maudhui kwenye tovuti au kuwasiliana kwa njia ya intaneti kwa kutumia baruapepe na kwa kutumia vikoa vya **.**tz ni usajili wa majina ya vikoa. Katika kutoa huduma zake, tzNIC inafuata mfumo wa rajisi - msajili – msajiliwa ili kukidhi mahitaji ya wateja wake kwa ufanisi na kwa ushindani. Mtindo huu unairuhusu tzNIC kutoa huduma za usajili sambamba na wasajili wengine kama ambavyo mashirika ya ndege yanavyotoa huduma ya usafiri wa anga sambamba na mawakala wake. Kwa sasa tzNIC ina wasajili watano (5) wanaotambulika kwa mujibu wa taratibu na kanuni zake. Wasajili hawa ni:

a) University Computing Centre (UCC);
b) Arusha Node Marie (Habari);
c) Simbanet (T) Ltd;
d) IT Farm Ltd na
e) Twigatech Ltd.

Kati ya wasajili hao, wanne wako Dar es Salaam na mmoja (Habari) yuko Arusha. Kwa hiyo, huduma za usajili wa majina ya vikoa vya **.**tz zinapatikana kwa urahisi kutoka tzNIC au kwa wasajili waliotajwa hapo juu. Gharama za usajili wa majina ya vikoa vya **.**tz zinaanzia Tsh.

5,000 hadi Tsh. 25,000 wakati ada ya matengenezo kwa mwaka inatofautiana kutoka Tsh. 5,000 hadi Tsh 20,000. Gharama hizi ziko sawa bila kujali unasajili kwa msajili yupi. Kwa kipindi cha kuanzia mwezi Mei mpaka Julai 2010, tzNIC imefuta gharama za usajili na hivyo basi itatoa usajili kwa gharama za ada ya matengenezo (renewal fee) tu.

Kwa sasa idadi ya majina ya vikoa vya **.**tz yanakaribia 5,500. Kutokana na ukweli kuwa tzNIC haitoi huduma zake kwa lengo la kutengeneza faida, gharama za baadaye za usajili na matengenezo zitategemea sana idadi ya majina ya vikoa vya .tz yatakayokuwa yamesajiliwa. Hivyo basi, wingi wa idadi ya majina ya vikoa vya **.**tz yatakavyokuwa yamesajiliwa ndiyo itakayotoa fursa ya kufikiria upya gharama za usajili.

Kutokana na thamani na hadhi ya majina ya vikoa vya **.**tz, tzNIC ingependa kufafanua masuala makuu mawili:

a) Usajili wa majina ya vikoa vya **.**tz
b) Kuhuisha (renew) majina ya vikoa vya **.**tz

a) Usajili wa majina ya vikoa vya .tz

Wakati twiga na mlima Kilimanjaro vinaiweka Tanzania kileleni katika masuala ya utalii, majina ya vikoa vya **.**tz yanabainisha na kukupa utambulisho wa pekee unaohusiana na Tanzania katika mtandao wa Intaneti. Kwa hiyo, Watanzania wote, shule, vyuo, biashara ndogo ndogo na za kati, kampuni, asasi za kiserikali na zisizo za kiserikali zinaombwa kusajili na kutumia majina ya vikoa vya **.**tz badala ya majina ya vikoa vya kawaida kama **.**org, **.**com, n.k.

Usajili na matumizi ya majina ya vikoa vya .tz unachangia maendeleo ya rajisi ya **.**tz (rasilimali ya Tanzania) kwa kuwa ada ya usajili na matengenezo inayolipwa inabaki hapa hapa nchini na kujenga weledi wa wazawa katika kuendesha na kusimaia rasilimali hii muhimu. Faida nyingine zinajumuisha:

i. Fursa ya kutoa taarifa kwenye Intaneti juu ya huduma unazotoa au biashara unayofanya;
ii. Mazingira sawa ya ushindani wa kimasoko bila kujali ukubwa wa kampuni husika;

iii. Ufanyaji kazi mzuri wa vitafuta taarifa (search engines) katika mtandao wa Intaneti;

iv. Utatuzi wa haraka na wa gharama nafuu wa matatizo yanayohusiana na usajili wa majina ya vikoa vya .tz unaozingatia taratibu, kanuni, desturi na sheria za hapa hapa nchini;

v. Uchangiaji katika kupunguza gharama za uunganishwaji katika mtandao wa Intaneti tokana na uwezekano wa mawasiliano mengi kutotoka nje ya nchi (content / traffic localization);

vi. Fursa za kuwafikia wateja ulimwenguni kote, kwa gharama nafuu na kwa wakati.

b) Kuhuisha (renew) majina ya vikoa vya.tz

Tanzania Network Information Centre (tzNIC) ilichukua jukumu la kutoa huduma ya usajili wa majina ya vikoa vya **.**tz tangu Agosti, 2009. Hii ilikuwa baada ya kuhamishia katika rajisi mpya majina yote ya vikoa vya .tz yaliyokuwa yamesajiliwa awali. Rajisi mpya ni ya mfumo wa malipo ya kabla. Hii inamaanisha kuwa jina la kikoa cha .tz linasajiliwa baada ya kulipia gharama za usajili na matengenezo (registration and maintenance fee). Matokeo yake ni kwamba jina la kikoa cha .tz ambalo muda wake wa matumizi unakuwa umekwisha na halijalipiwa gharama za matengenezo (renewal fee) kwa mwaka unaofuata, linaweza kusajiliwa na mtu mwingine. Usajili wa jina la kikoa ambalo muda wake unakuwa umekwisha unaweza kufanywa na mtu mwingine kwa lengo ama la kimapato au ushindani wa kibiashara. Hii ni kwa sababu jina la kikoa cha **.**tz lina thamani na kwa hiyo ni vema likalindwa.

Kuhuisha (renew) jina la kikoa ni moja ya hatua muhimu za kulinda jina la kikoa cha **.**tz. Kwa hiyo tzNIC inawaomba wamiliki wote wa majina ya vikoa vya **.**tz kuhuisha majina yao ya vikoa kabla muda wake kwisha (mwaka mmoja baada ya kusajili). Kwa wale ambao walisajili majina ya vikoa kabla tzNIC haijachukua jukumu la kusimamia usajili wa vikoa vya .tz (Agosti, 2009) wanakumbushwa kuhakiki kumbukumbu zote zinazohusiana na usajili na pia kuhuisha usajili huo kabla ya mwisho wa mwezi Julai 2010.

Ili kusaidia mchakato wa uhuishaji wa majina ya vikoa yaliyokwisha sajiliwa, tzNIC imeandaa jarida (linalopatikana hapa **http://www.tznic.or.tz/docs/domain_renewal_steps.pdf**) litakalotumiwa katika kampeni ya

uhuishaji. Jarida hili linaelezea hatua nne (4) rahisi ambazo msajiliwa anapaswa kuzifuata ili muda wa matumizi wa jina lake la kikoa cha .tz usiishe bila yeye kujua. Hatua hizo ni:

a) Uthibitishaji wa taarifa za usajili kupitia huduma ya **Whois** inayopatikana kwenye tovuti ya tzNIC – http://whois.tznic.or.tz/whois;

b) Uthibitishaji na uhakiki wa taarifa za mawasiliano ya kiutawala ili taarifa (notice) za rajisi zinazohusiana na kikoa husika zimfikie mlengwa;

c) Kuunganisha usajili wa majina ya vikoa vya **.**tz kwa msajili mmoja kwa ajili ya urahisi wa usimamiaji, na

d) Usajili wa majina ya vikoa vya .tz kwa kipindi kirefu (miaka mitano).

Mwisho tzNIC inawaomba watanzania wote kusajili majina ya vikoa vya .tz kwa ajili ya kampuni zao, bidhaa zao, huduma na majina ya biashara zao. Pia wasajiliwa wanahimizwa kuhuisha usajili wao kwa wakati muafaka ili kuepuka madhara ya kutofanya hivyo. Wadau wote wanaombwa kutumia kikamilifu kipindi hiki cha kampeni ya uhuishaji na promosheni ya usajili wa majina ya vikoa vya .tz.

Hakuna kinachoitambulisha Tanzania katika mtandao wa Intaneti kama .tz iwezavyo

Kuhusu tzNIC

Tanzania Network Information Centre (tzNIC) ni kampuni isiyotengeza faida iliyoanzishwa mwaka 2006 kwa madhumuni ya kusimamia na kuendeleza rajisi ya majina ya vikoa vya .tz. Kituo hiki kimesajiliwa kama kampuni kwa dhamana yenye ukomo. tzNIC inapania kuhamasisha matumizi ya majina ya vikoa vya tz; kukuza weledi katika kuendesha na kusimamia rajisi ya majina ya vikoa vya .tz; kulinda maslahi ya wasajiliwa na kuchangia katika ulinganifu wa sera za usimamizi wa rajisi ya .tz katika ngazi ya kitaifa na kimataifa. tzNIC inawezesha uundaji na upatikanaji wa habari maudhui kwenye Intaneti, kurahisisha upatikanaji wa majina ya vikoa vya .tz na kuwezesha utambulisho wa Tanzania kwenye mfumo wa Intaneti.
##

Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi:

LAPF Millenium Towers, Ghorofa ya Chini, Chumba Na. 04, S.L.P. 34543, Simu: (0)22 2772659,
Faksi (0)22 2772660, baruapepe: info@tznic.or.tz na manager@tznic.or.tz, Tovuti: www.tznic.or.tz

Imetolewa na:

Abibu R. Ntahigiye
Meneja, tzNIC.